

UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Abu Dhabi, Al Manhan
Al Walidain Street, Villa No. 31
Tel : +97126313088
P.O Box : 43714
E-mail : abudhabi@nje.go.tz



سفارة جمهورية تنزانيا المتحدة
أبو ظبي

EMBASSY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA ABU DHABI

TAARIFA KUHUSU MSAMAA WA MAKOSA YA UKAAZI NCHINI UMOJA WA FALME ZA KIARABU (UAE).

1. UTANGULIZI:

Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) imetoa kipindi cha msamaha wa makosa ya ukaazi nchini kwa miezi miwili kuanzia Septemba 1, 2024 hadi Oktoba 31, 2024. Mpango huu unatoa fursa kwa Raia wa kigeni wenye makosa yoyote ya ukaazi kurekebisha makosa yao na kuendelea kuishi nchini au kuondoka bila ya masharti. Watu wenye hali hii kama vile visa ziliokwisha muda au kupita (Overstayed) watapata fursa yakurekebisha hali hiyo au kurekebisha hadhi zao za kuishi nchini au kurejea Tanzania bila masharti.

Makundi yanayoweza kunufaika na msamaha huo nikama yafuatayo: -

- (a) Raia wa kigeni wenye vibali vya makazi vilivyokwisha muda au visa zilizokwisha muda.
- (b) Wafanyakazi wa ndani waliotoroka kwa waajiri wao na kupoteza paspoti zao.
- (c) Watoto waliokuwa wakiishi UAE lakini hawakurekodiwa ndani ya miezi minne/kutengenezewa vibali vya ukaazi.

Aidha, Unaweza kuhuisha visa yako au kuhamisha udhamini kwa mwajiri mpya bila kulipa faini. Maombi yanaweza kufanywa katika vituo rasmi kama vile vituo vya Amer mjini Dubai au vituo vya ICP mjini Abu Dhabi. Vilevile kwa wote watakaotaka kuondoka nchini wanaweza kufanya hivyo kwa kuomba kibali cha kutoka nchini UAE, na kufuata taratibu bila kutozwa faini.

2. UTARATIBU:

Unaweza kuomba msamaha kupitia:

- (a) **Binafsi:** Tembelea vituo vya Amer mjini Dubai au vituo vya ICP mjini Abu Dhabi, Al Dhafra, Sweihan, au Al Awir.
- (b) **Mtandaoni:** Tuma maombi yako kupitia mfumo wa huduma za smart ya UAE.

3. MAMBO YA KUZINGATIA:

- (a) Msamaha utadumu hadi Oktoba 31, 2024. Maombi ya kurekebisha hali na kutoka lazima yakamilishwe kabla ya tarehe hii.
- (b) Wale wanaochagua kuondoka UAE lazima waondoke ndani ya siku 14 baada ya kupokea kibali cha kutoka, vinginevyo faini na vikwazo vitarejelewa.
- (c) Ikiwa utashindwa kurekebisha hali yako au kuondoka baada ya tarehe ya mwisho ya msamaha, utakabiliwa na faini au adhabu za kisheria, ambazo zinaweza kujumuisha kuondoshwa nchini (Deportation).
- (d) Ikiwa pasipoti yako imepotea, kwanza toa taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nawe na kupata hati ya kupotea kwa pasipoti.
- (e) Wasiliana na Ubalozi wa Tanzania mjini Abu Dhabi au Ubalozi Mdogo uliopo Dubai ili kuomba pasipoti mpya au hati ya dharura ya kusafiria (ETD).
- (f) Mara upatapo pasipoti mpya, unaweza kurekebisha hadhi yako ya makazi au kuomba kibali cha kuondoka nchini UAE.

4. HITIMISHO:

Kufuatia taarifa hii, Ubalozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Abu Dhabi, unaomba na kuwasihi wale wote wenye matatizo yaliyo ainishwa hapo juu kuitumia fursa hii adhimu kurekebisha hadhi za ukaazi ili kuweza kuishi nchini UAE kwa mujibu wa taratibu na sheria za nchi.

11/9/2024

UBALOZI WA TANZANIA NCHINI UMOJA WA FALME ZA KIARABU